**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA
**WAKALA YA SERIKALI MTANDAO**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

## UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO NCHINI

### 1.0 Serikali Mtandao

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi za umma kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma na taarifa kwa Umma, kwa haraka na kwa gharama nafuu. Utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao imegawanyika katika maeneo makuu manne, ikiwa ni kati ya **Serikali na Watumishi** (G2E), **Serikali na Sekta ya Biashara** (G2B), **Serikali na Wananchi**(G2C) na **Kati ya Taasisi moja na Taasisi nyingine za Serikali** (G2G).

### 2.0 Malengo ya Serikali Mtandao

Serikali Mtandao ina malengo ya kuimarisha utawala bora na kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za Umma kwa kuhakikisha kuwepo kwa mawasiliano ya haraka, yenye uhakika na salama ndani na kati ya taasisi mbalimbali za Serikali kuanzia kwenye Wizara, Mikoa hadi ngazi za Halmashauri pamoja na Balozi zetu nje ya nchi na kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

Malengo mengine ni Kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi Serikalini, Kuimarisha usalama wa Serikali na raia wake katika karne ya sayansi na teknolojia na kuongeza uwezo wa Serikali kupambana na majanga kwa kutumia teknolojia ili kurahisisha michakato ya utendaji kazi katika taasisi za Serikali na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

### 3.0 Wakala ya Serikali Mtandao

Wakala ya Serikali Mtandao ilianzishwa Aprili 2012 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na.30 ya Mwaka 1997 Sura ya 245 na Kanuni zake. Wakala hii ina jukumu na mamlaka ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa Taasisi za umma. Lengo ni kuziwezesha Taasisi hizo kutumia TEHAMA katika majukumu yao ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

## 4.0 Malengo ya Wakala ya Serikali Mtandao

Malengo ya Wakala ya Serikali Mtandao ni pamoja na Kuboresha uwezo wa Taasisi za umma kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao, Kuboresha upatikanaji wa huduma mtandao kwa umma, Kuboresha mifumo shirikishi ya TEHAMA, Kuimarisha uratibu, usimamizi na uzingatiaji wa viwango vya Serikali Mtandao katika utoaji wa huduma kwa umma na Kuboresha huduma za ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi. Malengo haya yanaenda sambamba na misingi ya utekelezaji wa Serikali mtandao.

## 5.0 Mafanikio ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao

### 5.1 Uwezo wa Taasisi za umma kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao

Wakala inalenga kuinua uwezo wa wataalam wa TEHAMA kwa kuwapa maarifa na ustadi wa kubuni, kutengeneza na kutumia mifumo tumizi inayowezesha utoaji wa huduma kwa njia ya kompyuta au vitumi vingine. Mafunzo mbalimbali yametolewa kama ifuatavyo;

i) Mafunzo ya Usimamizi na Ujenzi wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini na Usalama wa Mtandao ambayo yametolewa kwa taasisi za umma **149** wakiwemo Maofisa TEHAMA **226** na bado yanaendelea kutolewa.

ii) Mafunzo ya Uendeshaji wa Vituo vya Data kwa Usalama yametolewa kwa Taasisi za umma **91** wakiwemo Maofisa TEHAMA **162.**

iii) Mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Barua Pepe Serikalini yametolewa kwa Taasisi **157.**

iv) Mafunzo ya usimamizi wa Taarifa za usimamizi wa Tovuti za serikali yametolewa Kwa taasisi **71**. Mafunzo ya uwekaji taarifa katika tovuti kuu yametolewa kwa taasisi **86**. Mafunzo hayo yanaendelea kutolewa kwa kila taasisi ambayo inatengenezewa Tovuti na Wakala.

### 5.2. Upatikanaji wa Huduma Mtandao kwa Umma

Wakala imetengeneza mifumo na tovuti mbalimbali kwa taasisi za umma ikiwa ni jitihada za kuziwezesha taasisi hizo kutoa huduma na taarifa mbalimbali za Serikali kwa wananchi kwa njia ya mtandao. Wakala pia imeimarisha miundombinu ya msingi kwa ajili ya utoaji wa huduma mtandao kwa umma kwa wakati, uwazi, urahisi na gharama nafuu.

Wakala imetengeneza mifumo tumizi kwa kazi maalum kama vile POLIS (wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania), Ajira Serikalini, Mfumo wa Wananchi wa kuwasiliana moja kwa moja na Serikali kwa masuala mbalimbali pamoja na Mfumo wa huduma za Serikali kupitia simu za Mkononi *152*00# ambao hutumiwa na taaasisi za umma katika

kuwahabarisha wananchi kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo huduma wanazozitoa na mfumo uliowezesha tume ya uchaguzi kuendesha zoezi lote la uchaguzi.

Aidha wakala imetengeneza tovuti mbalimbali ambazo ni pamoja na **Tovuti Kuu ya Serikali** (www.tanzania.go.tz) ambayo ni dirisha moja la kutolea huduma kwa umma, **Tovuti Kuu ya Ajira** (portal.ajira.go.tz) ambayo inatoa taarifa kuhusu nafasi zote za kazi zinazotangazwa Serikalini, Tovuti ya Wananchi, (www.wananchi.go.tz), Tovuti ya Takwimu Huria (www.opendata.go.tz), Ikulu, Tovuti ya Katibu Mkuu Kiongozi, Bunge, Bunge Maalum la Katiba na Tume ya taifa ya uchaguzi. Aidha, Wakala imetengeneza pia baadhi ya Tovuti za Wizara, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Majiji, Manispaa, Miji, Mamlaka, Bodi, Wakala, Shirika la Elimu Kibaha na Kampuni za Serikali

## 5.3 Rasilimali Shirikishi za TEHAMA

Wakala imeweka mazingira yanayowezesha taasisi za umma kushirikiana katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA ili kuondoa urudufu wa jitihada, kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na kuipunguzia Serikali gharama za kutengenezea kila taasisi mfumo wake pamoja na kuongeza ubora wa huduma kwa umma.

### 5.3.1. Mfumo wa Barua pepe Serikalini (GMS)

Kwa kufanikisha hayo, Wakala imetengeneza Mfumo wa Barua pepe Serikalini (GMS) kwa ajili ya taasisi za umma. Lengo likiwa ni kuimarisha mawasiliano kwa njia ya barua pepe na kuongeza usalama wa ubadilishanaji taarifa. Aidha mfumo huu umeunganishwa na Mfumo Shirikishi wa Rasilimali watu na Mishahara (HCMIS) ili kuhakikisha unabadilishana taarifa na mifumo mingine ya Serikali. Hadi sasa taasisi 117 zinatumia mfumo huu.

### 5.3.2 Vituo vya Kuhifadhi Mifumo ya Serikali

Serikali imejenga vituo vikuu vya kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali pamoja na kujikinga na majanga unaozingatia viwango vya Usalama vya kitaifa na kimataifa.

### 5.3.3. Utoaji Huduma za Serikali kupitia simu za Mkononi

Wakala imetengeneza Mfumo Shirikishi wa Utoaji huduma za Serikali kupitia simu za Mkononi. Mfumo huu unawarahisisishia wananchi kupata huduma za Serikali popote walipo na unaokoa muda wa kufuata huduma kwenye ofisi za Serikali na kupunguza gharama za kupata huduma husika, unapunguza urasimu usio wa lazima na kupunguza mianya ya rushwa.

Mfumo huu ambao umebeba huduma mbalimbali zitolewazo na taasisi za umma unapatikana kwa wananchi kupitia namba maalum ya kutolea huduma ***152*00#** na kwa taasisi za Serikali kupitia tovuti govsms.ega.go.tz na hivi sasa taasisi **22** za umma zimejiunga na kutumia mfumo huu.

### 5.3.4. Miundombinu ya Mawasiliano Serikalini (Govnet)

Wakala inasimamia miundombinu ya mawasiliano Serikalini (Govnet) inayowezesha taasisi za umma kuwa na mawasiliano ya kielektroni (data, sauti na video) ya ndani yenye usalama na gharama nafuu. Matumizi ya Mtandao huu yanaipunguzia serikali gharama za matumizi kwa njia ya mtandao wa data kwa zaidi ya **80%.** Hadi sasa, taasisi 72 za Serikali zikiwepo Wizara, Wakala za Serikali na Idara zinazaojitegemea zilizopo katika mikoa ya Dar es salaam, Dodoma na Pwani. Taasisi nyingine zikiwemo Mamlaka za Halmashauri za mitaa zinaendelea kuunganishwa.

### 5.3.5 Simu zinazotumia Itifaki ya Intaneti (IP PBX)

Wakala imeunganisha taasisi za umma 72 zikiwemo Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali kwenye mfumo wa zinazotumia intaneti kuziwezesha taasisi hizo kuwa na mawasiliano yaliyo bora, salama na kupunguza gharama za mawsiliano Serikali.

Taasisi hizo zimeunganishwa na Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali yaani 'Government Communication Network (Govnet)' unaouwezesha mfumo wa simu hizo kufanya kazi kwa ufanisi ambapo mtumishi wa taasisi moja katika taasisi hizo anaweza kupiga simu kwenda taasisi nyingine ya nje ikawa kama amepiga simu ya 'extension' ndani ya ofisi moja. Taasisi hizo zitaendelea kuwasiliana na taasisi zilizo nje ya mtandao huo kwa kupitia mtoa huduma wa simu za mezani (PSTN Provider) kama vile TTCL.

### 5.3.6. Matumizi ya Masafa ya Intaneti ya Serikali

Wakala inaratibu matumizi ya masafa ya intaneti yaliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya intaneti kwenye taasisi za umma. Huduma hii imewezesha Serikali kuokoa kati ya asilimia 50 hadi 90 ya gharama iliyokuwa unalipwa na Serikali kwa makampuni binafsi. Hadi sasa taasisi 176 zimeunganishwa na zinatumia masafa ya intaneti ya Serikali kwa ajili ya kuwezesha mawasiliano ya utendaji kazi.

## 6.0 Uratibu, Usimamizi na Uzingatiaji wa Viwango vya Serikali Mtandao katika Utoaji wa Huduma kwa Umma

Wakala inasimamia udhibiti wa viwango vya Serikali Mtandao kwa kutumia miongozo mbalimbali na viwango vilivyowekwa ili kuwa na mifumo bora ya TEHAMA.

### 6.1. Miongozo

Hadi sasa, Wakala imetoa miongozo inayotoa maelekezo na ufafanuzi wa taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika utekelezaji wa jitihada mbalimbali zinazohusu TEHAMA katika taasisi za umma.

Miongozo inayotumika kwenye taasisi za serikali ni pamoja na Orodha Hakiki ya Miradi ya TEHAMA, Vigezo vya Kuhakiki Miradi ya TEHAMA, Taratibu za Kuhakiki Miradi na Mwongozo wa Kusimamia Miradi ya Tehama Serikalini.

### 6.2. Viwango

Toleo la kwanza la kanuni, Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao vimekamilika na Viwango hivi vitatumiwa na taasisi za Serikali katika kuteleza jitihada za Serikali Mtandao. Miongozo na Viwango hivi vinapatikana kwenye tovuti ya wakala www.ega.go.tz

## 7.0 Huduma za Ushauri wa Kitaalam

Wakala ya Serikali Mtandao inatoa huduma za ushauri wa kitalaamu na msaada wa kiufundi kwa taasisi mbalimbali za umma. Taasisi za Serikali **42** zimepewa ushauri na utaalamu elekezi kuhusu kubuni, kutengeneza na kusimamia mifumo na miundombinu mbalimbali ya TEHAMA kwenye taasisi zao. Taasisi **135** zimepewa ushauri wa kawaida katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao

## 8.0 Hitimisho

Wakala ya Serikali Mtandao itaendelea kutimiza malengo iliyojiwekea ili kwenda sambamba na malengo ya Serikali Mtandao. Pia, Wakala imejizatiti katika kubuni mifumo mbalimbali itakayorahisisha utendaji kazi na kuziwezesha taasisi za umma kutoa huduma bora kwa wananchi na kwa wakati mwafaka huku ikiipunguzia gharama Serikali kupitia mifumo itakayobuniwa na kutengenezwa na wataalam wa ndani.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx **MWISHO** xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

**Imetolewa Na:**
**Suzan Mshakangoto**
**MENEJA HABARI, ELIMU NA MAWASILIANO**
**WAKALA YA SERIKALI MTANDAO.**